34

# MKATABA KUWEKA TERRAZZO MAJENGO MBALIMBALI.

KATI YA

CHUO CHA MAFUNZO YA UFUNDI STADI
(VETA MANYARA)

NA

ALBERTO BONIFACE ZAKARIA LULANDALA

NOVEMBER, 2021

## A: MASHARTI MAALUM YA MKATABA

<table>
<tr><td>1</td><td>MWAJIRI</td><td colspan="3">Mkuu wa Chuo<br>VETA Manyara<br>S. L. P 485 Babati</td></tr>
<tr><td>2</td><td>JINA NA ANWANI YA FUNDI (Mwajiriwa)</td><td colspan="3">Jina: ALBERTO . BONIFACE Z-LULANDALA<br>Anwani: P.O. BOX 10324, ARUSHA<br>Simu: 0717 847520</td></tr>
<tr><td>3</td><td>ENEO LA UJENZI</td><td colspan="3">Monduli-Arusha</td></tr>
<tr><td rowspan="2">4</td><td rowspan="2">MAELEZO YA KAZI KWA UFUPI</td><td colspan="3">JENGO: COMPUTER LAB.AND SECRETARIAL WORKSHOP</td></tr>
<tr><td>i</td><td>KUWEKA TERAZO@M² 25,000/= (409.08M²)</td><td>10,227,200/=</td></tr>
<tr><td>5</td><td>GHARAMA YA UFUNDI NA VIFAA (MATERIALS):</td><td colspan="3">10,227,200/=</td></tr>
<tr><td>6</td><td>MUDA WA MKATABA<br>(Tangu Kusainiwa kwa Mkataba): siku 21</td><td colspan="3">Tarehe ya Kusaini: 27/11/2021<br>Muda: Siku 88<br>Tarehe ya Kuanza Kazi 29/11/2021<br>Tarehe ya Kumaliza Kazi 28/02/2022</td></tr>
<tr><td>7</td><td>MASHARTI YA MALIPO:</td><td colspan="3">• Hakuna Malipo ya Awali<br>• Fundi atalipwa kwa awamu 2 (50% baada ya kuanza kazi na 50% baada ya kazi husika kukamilika na kukaguliwa.</td></tr>
</table>

Principal
VETA Manyara RVTSC
P.O. Box 485
BABATI

## B: MASHARTI YA JUMLA MKATABA

1. Fundi ataleta vifaa vyote vinavyohitajika kwa ajili ya uwekaji Terrazzo kulingana na mahitaji katika kila jengo ambavyo vitakaguliwa na mhandisi msimamizi wa site na kuthibitisha ubora hitajika.
2. Fundi atafanya kazi kwa mujibu wa mchanganuo wa kazi na mwongozo wa Mtaalamu Mshauri, kwa umakini na uhodari wa hali ya juu wa kiufundi.
3. Fundi asipofanya kazi yake vizuri, Mwajiri ana haki ya kumsimamisha kazi na kulipa hasara zote zilitokana na uzembe au makusudi.
4. Fundi atatoa maelekezo ya kazi kwa vibarua wake na atahusika moja kwa moja kwenye ujenzi kwa kutumia vibarua wake na kuwaunganisha mafundi wote aliowaajiri kuhakikisha kazi inafanywa kulingana na taratibu za uwekaji tiles.
5. Fundi kwa wakati wote anatakiwa kuhakikisha yeye pamoja na mafundi wake wanazingatia nidhamu na tabia njema na asiajiri kabisa mtu asiyekuwa na utaalumu au ujuzi wa kutosha.
6. Fundi atahusika na vitendo *(kama wizi, uharibifu wa mali za chuo)* vyote vinavyofanywa na mafundi wake na mtu yeyote anayefanya kazi chini ya usimamizi wake.
7. Fundi kwa wakati wote ahakikishe kuwa eneo la kazi linakuwa safi na salama na pia pindi kazi iishapo ahakikishe vifaa vyote vilivyosalia katika eneo la upauzi kama mabaki vimewekwa sehemu husika na kuacha eneo likiwa safi na salama.
8. Kiasi cha asilimia 11% ya kiasi cha mkataba kitashikiliwa na Mwajiri kwa muda mpaka kazi kukamilika na kukaguliwa na kujiridhisha *(Retention Money)* na kulipwa mara baada ya ukaguzi wa mwisho kufanyika.
9. Malipo yoyote yanayolipwa yatakatwa kodi ya serikali kama sheria inavyoelekeza.

Principal
VETA Manyara RVTSC
P.O. Box 485
BABATI

10. Ucheleweshaji wa Kazi:

- Ucheleweshaji wa kazi uliosababishwa na fundi, fundi atapewa adhabu ya kulipa kiasi sawa na hasara iliotokana na ucheleweshwaji huo.

11. Ucheleweshaji wa Vifaa na Malipo:

- Ucheleweshaji uliosababishwa na Mwajiri *(kutokana na fedha au vifaa)*, Fundi ataongezewa muda wa kumalizia kazi.

12. Uvunjwaji wa Mkataba:

- Mkataba utavunjwa iwapo; Fundi au Mafundi walioko chini yake au vibarua wake watajihusisha na wizi wa vifaa vya ujenzi au mali yoyote ya Chuo.

- Mkataba utavunjwa iwapo; Fundi au Fundi wake hatazingatia taratibu za uwekaji terrazzo au ubora wa kiufundi katika kazi yake, ikiwemo kufuata michoro au maelekezo ya Mtaalamu Mshauri.

**MWAJIRI:**

Saini:................................ Principal VETA Manyara RVTSC P.O. Box 485 BABATI

Jina: FELIX S. OLEN

Cheo: MKUU WA CHUO

Tarehe: 27.11.2021

**FUNDI:**

Saini:..............................

Jina: ALBERTO B. ZAKARIA LULANDLA

Cheo: FUNDI

Tarehe : 27/11/2021

**SHAHIDI WA MWAJIRI**

Saini: ..................................

Jina: THULNAT NZOWA

Cheo: K/MSA SIU

Tarehe: 27/11/2021

**SHAHIDI WA FUNDI**

Saini..................................

Jina: ASHUMAN MJATA

Cheo: FUNDI

Tarehe: 27/11/2021